

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA

08 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SABA – TAREHE 08 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

387. **MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ina upungufu wa Walimu wa Shule za Msingi takribani 1,270 kwa mujibu wa Ikama:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Walimu katika Halmashauri hiyo.

388. **MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):

Je, ni lini Serikali itanza kutoa Elimu ya ujasiriamali kwa Wanawake na Vijana wanaopewa Mikopo ya asilimia 5 katika Halmashauri Nchini.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

389. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni kwa nini Askari Polisi wasiwekewe utaratibu wa kusamehewa Kodi katika vifaa vya ujenzi na kupewa Viwanja kwa bei elekezi ili wawe na moyo wa kulitumikia Taifa bila kujiingiza katika njia za udanganyifu kwa lengo la kujiandaa na maisha baada ya kustaafu.

WIZARA YA KILIMO:

390. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Bonde la Mto Ruhuhu lililopo Kata ya Lituhi linawanufaisha Wananchi kwa kuweka miundombinu ya Kilimo cha umwagiliaji.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

391. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ipo tayari kuunga mkono juhudi za Wananchi wa Kata ya Makata – Liwale ambao wameanzisha ujenzi wa Chuo cha VETA na madarasa mawili yameshakamilika.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

392. MHESHIMIWA ALAUDIN HASHAM SALIM (ULANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Mahenge utaanza kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020.

393. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Singida ili ndege za ATCL zianze kutua na kurahisisha usafiri.

**394. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU
(ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Mhe. Rais ya ujenzi wa Barabara ya Mianzini, Sambasha, Ngaramtoni hadi Hospitali ya Seliani kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**395. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO
(MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni nini mpango wa Serikali wa kukamilisha ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi ambao umeanza tangu Mwaka 2008/2009 bila kukamilika.

**DODOMA
08 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**